

CREATING HOPE IN CONFLICT: A HUMANITARIAN GRAND CHALLENGE



Picha Kwa Hisani Ya: Sehat Kahani

KUTUHUSU

Kuleta Matumaini katika Mizozo: Ushirikiano katika Usaidizi wa Kibinadamu ni ushirikiano kati ya Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, Jumuiya ya Madola na Ofisi ya Maendeleo (FCDO), Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, Idara ya Masuala ya Kimataifa Nchini Canada, na Grand Challenges Canada.

Tunatafuta uvumbuzi thabiti, unaokoa maisha au kuboresha maisha; ambao unakidhi vyema mahitaji ya watu walio hatarini zaidi na watu walioathiriwa na majanga ya kibinadamu yanayosababishwa na mizozo; ambao ni vigumu kuwafikia.

WITO WA OMBI LA MAPENDEKEZO YA MIRADI YA KUFADHILIWA

Tunatafuta mapendekezo ya miradi ya kufadhilliwa kwa mara ya kwanza kutoka kwa mashirika ya ndani, watafiti, wavumbuzi, wasomi, na sekta ya kibinagsi; ambayo yanalenga kutatua changamoto sugu zaidi zinazowakabili watu wanaoishi katika maeneo yenye mizozo, wakimbizi wa ndani na wakimbizi. Uvumbuzi lazima uhusishe maoni kutoka kwa jamii zilizoathiriwa wanazotaka kuhudumia, na upendeleo utatolewa kwa suluhisho zinazomilikiwa na wenyeji.

Ufadhilli wa Dola za Canada za \$250,000 kwa uvumbuzi wa kwanza utatolewa kwa waomba ufadhilli watakaofaulu. Watakaopokea ufadhilli pia watapata usaidizi unaoendelea, rasilimali, ufikiaji wa mitandao, na fursa ya kushirikiana na wavumbuzi wengine wanaoshughulikia changamoto zinazofanana.

MAENEKO MAKUU YANAYOLENGWA

Nishati: Tunatafuta uvumbuzi thabiti wa kuzalisha nishati. Tuna haja hasa na ubunifu unaowezesha upatikanaji sawa na wa bei nafuu kwa suluhisho za mabadiliko ya tabianchi na/au bidhaa au huduma za nishati mbadala kwa watu walio katika mazingira magumu zaidi walioathirika na mizozo.

Taarifa za kuokoa maisha: Tunatafuta uvumbuzi unaoboresha uaminifu na usalama wa taarifa muhimu au za kuokoa maisha na/au kuboresha mawasiliano ya njia mbili.

Bidhaa na huduma za afya: Tunatafuta uvumbuzi unaoshughulikia vizuizi vinavyohusiana na miundombinu duni ya huduma za afya, ujuzi wa wafanyakazi wa afya, na mapungufu ya ufuatiliaji wa magonjwa yaliyopo na mwitikio uliopo.

Tuma ombi leo kwenye: humanitariangrandchallenge.org/rfps/